NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## Kikao cha Hamsini na Tisa – Tarehe 27 Juni, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango Kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 *(The Finance Bill, 2018)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):**

Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 *(The Finance Bill, 2018)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu

**NDG. PAMELA PALLANGYO–KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Tutaanza na Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki. Allan Kiula ni Mbunge wa Iramba Mashariki?

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba.

**NAIBU SPIKA:** Mbunge wa Mkalama, kwa niaba yake Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mashariki.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Monko ni Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini. Naomba sasa kwa niaba ya wananchi wa Mkalama swali la Mheshimiwa Kiula lipate majibu.

Na. 496

**Changamoto zilizoko katika Vituo vya Afya vilivyoko Wilaya ya Mkalama**

**MHE. JUSTIN J. MONKO (K.n.y MHE. ALLAN J. KIULA)** aliuliza:-

Wilaya ya Mkalama ina vituo vya afya vitatu ambavyo vinakabiliwa na changamoto za uhaba wa watumishi, vipimo, majengo huku idadi ya wakazi wanaohitaji huduma ikiongezeka:-

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza idadi ya watumishi wa kada zote za kitaaluma katika vituo hivyo?

(b) Je, ni lini Serikali itazipandisha hadhi zahanati kubwa ziwe Vituo vya Afya ili kuhudumia wananchi wengi zaidi kutoka Iguguno, Ilanda Msiu na Mkiko?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Allan Kiula, Mbunge wa Mkalama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imeajiri watumishi wa afya 2,534 kwenye hospitali za Wilaya, vituo vya afya na zahanati nchini. Kati ya hao, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ilipata watumishi 12. Vilevile Serikali inakamilisha ajira za watumishi wa afya 6,018 ambao wataajiriwa katika hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati. Maeneo yenye upungufu vikiwemo Vituo vya Afya vya Mkalama vitawekwa katika kipaumbele cha kupatiwa watumishi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kuboresha vituo vya afya vilivyopo ili viweze kutoa huduma bora kwa wagonjwa badala ya kupandisha hadhi zahanati zilizopo. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Serikali imejenga Kituo cha Afya Kinyambuli kilichogharimu shilingi milioni 400 ili kuboresha huduma za dharura na upausuaji kwa mama wajawazito.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin Monko, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, ni kweli Serikali imeweza kufanikiwa kujenga kituo kama alivyosema kilichogharimu shilingi milioni 400 katika Wilaya ya Mkalama, lakini Wilaya ile inahitaji vituo vingi vya afya na yapo majengo ambayo wananchi tayari wameshaanza kuyajenga na yamefikia katika kiwango cha kupaua. Je, Serikali iko tayari sasa kuja kukamilisha kituo kingine cha afya ili wananchi waweze kupata huduma bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Jimbo la Singida Kaskazini tunavyo vituo viwili vya afya. Kituo cha Mgori na Kituo cha Ilongero na vituo hivi havijapata fedha za ukarabati na havifanyi upasuaji ukizingatia kwamba Halmashauri yangu haina hospitali. Je, Serikali iko tayari sasa kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha vile vituo vianze kutoa huduma ya upasuaji na wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini waweze kupata huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ambao uko dhahiri na sisi Waheshimiwa Wabunge wote ni mashuhuda jinsi ambavyo Serikali imetilia maanani suala zima la afya kwa maana ya kujenga vituo vya afya pamoja na hospitali za Wilaya pamoja na kuziboresha Hospitali za Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu hii kasi ambayo tumeianza siyo ya nguvu za soda, tutaendelea nayo kuhakikisha kwamba tunaboresha masuala mazima ya afya ikiwemo katika Jimbo la Mkalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Monko ni shuhuda kwamba hivi karibuni Kituo chake cha Afya cha Mgori kimepelekewa pesa. Hii yote ni kuonesha jinsi ambavyo Serikali inajali afya za wananchi na jinsi ambavyo inaboresha huduma za afya. Naomba awe na subira kwa kushirikiana na Serikali hakika tutapiga hatua mbele zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, utusaidie na la kufuatilia haya majina, kwa sababu Iramba Mashariki Mbunge anajiita Mbunge wa Mkalama na anajijua hivyo na huwa anasema wananchi wa Mkalama sasa huku ikiitwa

Iramba Mashariki kidogo inaleta shida. Nadhani tatizo hilo liko pia upande wa Uyui bado wanaitwa Tabora kitu kama hicho. Kwa hiyo, mtusaidie majina yabadilishwe ili kumbukumbu zetu ziwe zinakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nami kuniruhusu niulize swali la nyongeza kwenye swali hili 496. Kwa vile Jimbo zima la Tabora Kaskazini lina kituo kimoja tu cha afya na Mheshimiwa Rais alipopita katika Jimbo langu aliambiwa tatizo hili na akachangia shilingi milioni 10 ili kujenga Kituo cha Afya pale Mwagelezi na Mbunge akachangia shilingi milioni tano. Je, Serikali iko tayari kutuongeza hela ili kituo kile kikamilike?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kwa dhati kabisa nipongeze juhudi ambazo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akizifanya kwa kushirikiana na wananchi wake. Jana tumepokea barua yake ambayo inaonesha jinsi ambavyo amechangia kutoka Mfuko wa Jimbo na pia katika kutoka vyanzo vyake katika suala zima la kuhakikisha afya inaboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie, kwa jitihada na nguvu ambazo ameanzisha pamoja na wananchi wake, kwa kadri nafasi itakavyoruhusu na bajeti ikiruhusu hakika hatutasahau kuhakikisha kwamba tunapeleka huduma ya afya. Kama ambavyo amekuwa akisema kwamba siku hizi mzigo mzito humbebeshi Mnyamwezi unampunguzia unataka kila mtu abebe wa kwake, naomba nimhakikishie kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma ya afya Uyui inaboreshwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuuliza swali kwenye Wizara hii. Mheshimiwa Naibu Waziri atakumbuka wakati wa ziara ya Waziri Mkuu Jimbo la Ndanda kwa maana ya Mkoa wa Mtwara alitembelea Kituo cha Afya cha Chiwale ambacho alikizindua siku ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote, Kituo cha Afya cha Chiwale kina uhaba mkubwa sana wa watumishi na barua tulishaipeleka toka mwezi wa Tatu kwa Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Mkuchika, nafikiri kwa kushirikiana na idara yake na Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema, pamoja na kufungua kituo kile cha afya mara moja atahakikisha watumishi wameletwa pale kwa ajili ya kupunguza tatizo lililoko pale. Je, ni lini sasa Wizara itapeleka hao watumishi Kituo cha Afya cha Chiwale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna suala zima la upungufu wa watumishi kwa upande wa afya na hivi karibuni Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetangaza nafasi kwa ajili ya kuajiri watumishi wa afya ili kujaribu kupunguza pengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mchakato uko kwenye hatua za mwisho kabisa, haitapita mwezi kazi hii itakuwa imeshakamilika. Namwomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika maeneo ambayo kuna upungufu mkubwa tutazingatia kuhakikisha kwamba watumishi wanapalekwa ikiwa ni pamoja na kituo chake cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose Matembe, swali la nyongeza.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Iramba ina changamoto kubwa hususani kwa watumishi na vifaatiba. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka haraka watumishi na wataalam katika afya ya uzazi wa mpango?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake Mkoa wa Singida wamekuwa wakipigania suala zima la afya na jana nimejibu swali la Mheshimiwa Mbunge huyu ambaye leo ameuliza swali la nyongeza. Naomba nimhakikishie, kama nilivyotoa majibu alivyouliza Mheshimiwa Mwambe, mchakato wa ajira uko kwenye hatua za mwisho na lengo ni kuhakikisha kwamba maeneo yale yote ambayo yana upungufu yanapelekewa watumishi. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, zoezi likikamilika tutapeleka watumishi wa upande wa afya ili kupunguza hizo changamoto.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia, swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Miaka mitatu mfululizo iliyopita Madaktari wamekuwa wakihitimu vyuo vyetu vikuu vya humu ndani. Madaktati wako wanasubiri ajira na sekta ya afya ina upungufu wa zaidi ya asilimia 50 ya Madaktari katika vituo mbalimbali na sekta nzima. Je, kwa nini Serikali isi-*fast truck* ili Madaktari hawa walioko mitaani wakaingia kwenye utumishi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba tuna uhitaji mkubwa wa Madaktari, lakini pia atakubaliana na mimi kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetangaza nafasi na kama hilo halitoshi na Wizara ya Afya nayo imetangaza nafasi kwa ajili ya hao Madaktari na Wauguzi kwa ujumla wake. Naomba nimhakikishie kwamba mchakato upo pazuri, kwa hiyo, hicho ambacho anaulizia kuhusiana na suala zima la ku-*fast truck* ingekuwa tumechelewa wakati ule lakini kwa sasa hivi tuko hatua za mwisho, naomba avute subira hili litakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake

Na. 497

**Ahadi ya Ujenzi wa Jengo la Upasuaji *(Theatre)* na Vifaa vya Upasuaji – Lusewa na Namtumbo**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga *theatre* pamoja na vifaa vyake vya upasuaji katika Wilaya ya Namtumbo, Mji Mdogo wa Lusewa. Ahadi hii ni ya muda mrefu na wananchi wamekuwa wakiteseka kutokana na ukosefu wa huduma hiyo jambo ambalo limesababisha vifo hasa kwa akinamama wajawazito na watoto:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi huo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba ya Daktari katika Kituo cha Afya cha Lusewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Lusewa ulianza mwaka 2015. Ujenzi uliendelea katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo fedha zilipelekwa moja kwa moja kwenye akaunti ya kituo. Jengo la *OPD* limekamilika isipokuwa sakafu ya chumba cha upasuaji. Kituo hicho kitawekwa katika kipaumbele na kutengewa bajeti katika mwaka wa fedha 2019/2020 ili kukamilisha ujenzi unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ili kuboresha huduma za afya kwa mama na mtoto, Serikali imeweka kipaumbele na kutoa jumla ya shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya nane katika Mkoa wa Ruvuma ambapo kati ya fedha hizo, shilingi milioni 900 zimetolewa kwa vituo viwili vya afya vilivyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ambavyo ni Kituo cha Afya Msakale na Matemanga. Vituo vingine vilivyopokea fedha katika Mkoa wa Ruvuma ni Kalembo (shilingi milioni 500), Mkili (shilingi 400), Namtumbo (shilingi milioni 400), Madaba (shilingi milioni 400), Mahukuru (shilingi milioni 500) na Mchangimbole (shilingi milioni 500).

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati huu wa Serikali unalenga kuimarisha huduma za dharura na upasuaji kwa mama wajawazito.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali ambayo kimsingi yameacha kujibu kipengele (b), sasa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Lusewa ni Mji Mdogo ambao sasa hivi umeshapandishwa hadhi na

kuwa Mji Mdogo. Ni eneo ambalo lina wakazi wengi sana. Kutoka Lusewa kwenda Nalasi kuna umbali wa kilometa 150 na kutoka Lusewa kwenda Songea Mjini kwenye hospitali ya rufaa kuna kilometa 150. Wanawake wenzangu wa eneo hilo la Lusewa katika Mji Mdogo wamekuwa wakipata shida sana hasa kwenye suala la usalama wao wa uzazi na usalama wa mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake na watoto wamekuwa wakipoteza maisha na siku moja nilisimama hapa katika Bunge lako Tukufu nilionesha hisia zangu kwamba imefika mahali sasa kumtoa mwanamke kwenye Kituo hiki cha Lusewa ambacho hakina *theatre* kumpeleka Nalasi kilometa 150, gari la kubebea hao wagonjwa hakuna, wakati mwingine ni mabovu. Naomba Serikali inipe majibu ya kina ni lini itakamilisha ujenzi wa kituo hiki cha afya pamoja na kuweka hii *theatre* ambayo itawasaidia akinamama hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, *anyway* siyo swali lakini ni ombi, niseme kwamba, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami pamoja na Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, Mkurugenzi wa Namtumbo na *DMO* wa Namtumbo ili aende akaone mwenyewe kwa macho jinsi ambavyo wanawake wanavyopata tabu na watoto wanapoteza maisha katika maeneo yale?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi kwamba ujenzi wa kituo kile cha afya umekamilika isipokuwa chumba cha upasuaji kilichobaki ni sakafu peke yake. Naomba nitumie fursa hii kumuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ahakikishe kwamba katika vyanzo vyake vya

mapato kwa kushirikiana na wananchi kazi ya kumalizia sakafu iweze kukamilika ili wananchi waendelee kupata huduma badala ya kusubiri mpaka hicho kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Naamini kabisa katika vyanzo vyao vya mapato wakijibana wanaweza kumalizia kabisa suala zima la sakafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameomba mimi kuambatana na Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo. Naomba nimhakikishie, katika maeneo ambayo nina deni la kwenda kujionea mimi mwenyewe ni pamoja na Mkoa wa Mtwara lakini nikitoka Mtwara nitakuwa naenda Ruvuma halafu nitakwenda Njombe. Ilikuwa niende kwa bahati mbaya nikawa nimepatwa na msiba. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Susan Lyimo, swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahadi ni deni na kwa vyovyote vile Ilani hutekelezwa ndani ya miaka mitano, imekuwa ni kawaida kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi mara nyingi haitekelezwi siyo tu kwenye masuala ya afya ni pamoja na barabara na elimu. Nataka kupata kauli ya Serikali, je, hizi ahadi zao hasa za Marais zinakuwa ni za kuwadanganya watu? Pia ni lini sasa ahadi zote kuanzia zile za Mheshimiwa Mkapa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, ni swali la nyongeza unauliza moja. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili ambalo linaulizwa leo halina tofauti kabisa na ambalo aliuliza Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kuhusiana na ahadi za wagombea Urais na utekelezaji wa Ilani ya CCM. Katika majibu yangu ambayo nilitoa siku ile

nilieleza kwamba ahadi zimekuwa zikitekelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakishukuru jinsi ambavyo ahadi zinatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ahadi za wagombea Urais ndiyo mkataba wao na wananchi na wananchi wamekuwa wakiwapigia kura kwa ku-*base* kwenye hizo ahadi ambazo zinatolewa na Ilani ya CCM inatekelezwa ndani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa sababu amekuwa anafuatilia utekelezaji wa Ilani ya CCM na yeye mwenyewe anaamini kwamba tunatekeleza. Sasa amesema haitekelezwi, nadhani hapo atakuwa amepitiwa. Akatazame yale tuliyoahidi mangapi tumetekeleza, suala zima la afya yeye mwenyewe ni shuhuda na juzi tulikuwa tunaongea naye kuhusiana na barabara ya kule kwake na kazi imeshaanza kufanyika, kwa hiyo tunatekeleza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Ungando, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza; Kituo cha Afya Kibiti kimezidiwa, je, ni lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa ikizingatia pale hakuna *X-ray,* nyumba za wagonjwa na maabara ya uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, huyo ni Mwenyekiti wa Wandengereko, kwa hiyo, mletee majibu yake, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ungando, Mwenyekiti wa Wandengereko ambaye kwa mara ya kwanza amenipandisha boti nikaenda *Delta*, sehemu ambayo unaambiwa kwamba ikifika muda fulani maji

yakikauka inabidi usibiri saa nne. Nimefika kule na naomba nimpongeze jinsi ambavyo anapigania wananchi wa Jimbo lake la Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri kazi ambayo tulienda kusimamia sasa inakwenda vizuri. Kuna mambo ya hovyo yalikuwa yanafanyika katika ujenzi wa kituo kile cha afya lakini hata jana nilikuwa naongea na Mwenyekiti wa CCM ambaye alikuwa Mbunge, Ndugu Jabir Marombwa amenihakikishia ujenzi unakwenda vizuri. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, eneo hilo ambalo hakuna *X-ray* tayari tumeshapeleka pesa *MSD* kwa ajili ya vifaa, kwa sababu tunataka vituo vya afya vikamilike kwa kuwa na vifaa pamoja na wataalam ili vitoe huduma iliyokusudiwa kwa wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Julius Kalanga, swali la nyongeza.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na upungufu wa watumishi katika sekta ya afya lakini maslahi ya watumishi katika sekta ya afya yamekuwa duni hasa *on call allowance* ambayo Serikali kwa muda mrefu sasa haijapeleka fedha hizo katika *OC*. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo ili kusaidia Madaktari kufanya kazi zao kwa ufanisi?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo ninavyoongea katika maeneo yote ambayo kumekuwa na hamasa kubwa wananchi wakajiunga na *CHF*, hakuna tatizo la Madaktari kulipwa *on call allowance*. Akitaka kuchukua mfano, nimeenda Tanga pale sasa hivi katika hizi pesa ambazo wananchi wanachangia kwa kujiunga na Bima ya Afya, kulipana *on call allowance* si tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba Mheshimiwa Mbunge ahamasishe maeneo ya kwake wananchi wajiunge na Bima ya Afya na michango ile ambayo inatolewa ya 'Papo kwa Papo, Tele kwa Tele' hakika katika maeneo yote ambayo nimepita tangu utaratibu huu umeanza, kulipana *on call allowance* siyo tatizo tena.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, sasa aulize swali lake.

Na. 498

**Bajeti kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe iliweka kiasi cha shilingi bilioni 1.5 katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuanza kujenga hospitali ya Wilaya. Hata hivyo, kutokana na ukomo wa bajeti uliowekwa, fedha hiyo iliondolewa katika bajeti:-

Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fungu maalumu kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe iliweka kipaumbele na kutenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe lakini kutokana na ukomo wa bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 bajeti hiyo

haikupatikana. Hata hivyo, Serikali imetoa shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo viwili vya Afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ambavyo ni Iboya kilichopokea shilingi milioni 400 na Kituo cha Afya Masumbwe kilichopokea shilingi milioni 400 pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, katika Mkoa wa Geita, Serikali imeweka kipaumbele na kuanza ujenzi wa Hospitali za Wilaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale ambapo zimetengwa jumla ya shilingi bilioni tatu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, swali la nyongeza.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, Wilaya ya Mbogwe pamoja na Mikoa ya Kanda ya Ziwa tuna matatizo makubwa sana ya huduma za afya, matokeo yake wananchi walio wengi wanategemea sana huduma za waganga wa jadi na huko wakati mwingine wanapata uchonganishi na kuuana. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuwajengea wananchi wa Mbogwe Hospitali yao ya Wilaya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pamoja na kuipongeza Serikali kutupatia shilingi milioni 800 kwa ajili ya vituo vya Afya vya Iboya na Masumbwe. Je, Serikali iko tayari sasa kutupatia wataalam zaidi pamoja na vifaatiba?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Mikoa ya Kanda ya Ziwa pale ambapo huduma ya hospitali inakosekana

wamekuwa wakitumia tiba mbadala na kwa Mheshimiwa Mbunge imekuwa ni jambo la kawaida. Hata hivyo, sasa hivi tangu Serikali kwa kushirikiana na wananchi wameanza zimeanza kujengwa zahanati pamoja na vituo vya afya, naamini *mentality* imeenda iki-*change.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilienda Jimbo la Itilima kwa Mheshimiwa Silanga nikakuta kuna zahanati nyingi sana ambazo zimejengwa kwa kushirikisha wananchi na mwitikio ni mkubwa sana. Naomba hiyo kazi nzuri ambayo wameanza wenzetu wa kule ni vizuri na Mheshimiwa Mbogwe na yeye akaiga mfano mzuri ili wananchi wetu wahame katika tiba mbadala ambayo imekuwa ikisababisha mpaka watu kuuana kwa sababu ya masuala mazima ya kupiga ramli.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili juu ya suala zima la kupeleka wataalam, naomba nimhakikishie kwamba baada ya mchakato kukamilika wameajiriwa wataalam hakika na yeye mwenyewe anakiri kwamba tumempelekea vituo viwili vya afya. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba na wataalam wanapelekwa ili vituo vya afya vifanye kazi iliyokusudiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhary Raphael Michael, swali la nyongeza.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tatizo la Hospitali ya Wilaya lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ni sawa na tatizo la Hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi. Tayari Hospitali ya Mawenzi imezidiwa na wagonjwa kama Hospitali ya Mkoa na Manispaa ya Moshi kwa muda mrefu imekuwa na ombi hilo la Hospitali ya Wilaya ambalo tayari Serikali imeonekana imelikubali. Je, ni lini Serikali sasa italeta fedha ili hiyo Hospitali ya Wilaya ya Manispaa ya Moshi iweze kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo ambayo Hospitali za Wilaya hazipo zinaenda kujengwa na ndiyo maana tumeanza na hospitali 67. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya kwamba hizo 67 kukamilika hatutaishia hapo tutaenda maeneo mengine ambayo hakuna Hospitali za Wilaya ili tuweze kujenga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika juhudi za kuboresha huduma za afya katika Jimbo la Bagamoyo, wananchi katika Kata mbalimbali zikiwemo Nianjema, Fukayosi na Mapinga wameanza ujenzi wa zahanati katika vijiji vyao. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu kuwaunga mkono kumalizia ujenzi wa zahanati hizi?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu naomba kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa maana katika vituo vya afya vilivyojengwa vya kupigiwa mfano ni pamoja na Kituo chake cha Afya cha Bagamoyo. Naomba na wengine wa mikoa ya jirani ambao vituo vya afya vinaendelea kujengwa wakatazame mfano mzuri jinsi ambavyo walivyosimamia na *value for money* ikaonekana katika Kituo cha Afya cha Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo Serikali imekuwa ikiwaunga mkono maeneo mengine katika Jimbo lake, tukimaliza hatua hii, kama ilivyo kwenye Ilani ya CCM kwamba tunahakikisha tunajenga zahanati kila kijiji na

kituo cha afya kila kata, naomba tuvute subira hicho ndicho ambacho ni ahadi yetu sisi kwa wananchi, tutaenda kutekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Said Kubenea, swali la nyongeza.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuulizwa swali la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali nyingi za Wilaya kama Hospitali ya Sinza, Dar es Salaam ambayo ilikuwa Kituo cha Afya cha Sinza Palestina kimepandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya. Hata hivyo, hospitali hiyo haipati fedha kama Hospitali ya Wilaya na kukosekana kwa fedha hizo kumesababisha hospitali kushindwa kukidhi mahitaji yake ikiwemo kuwa na chumba cha kuhifadhia maiti. Je, Serikali iko tayari kupeleka fedha za Hospitali ya Wilaya katika Hospitali ya Sinza Dar es Salaam?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kila siku hii hospitali inaulizwa na majibu naona huwa yanatoka, sijui kama ni huwa hayasikiki humu ndani, hebu yaseme kwa namna ambayo hii Palestina utakuwa umemaliza leo, kwa sababu kila siku inaulizwa hii Hospitali ya Palestina. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kukumbusha kwamba swali hili limekuwa likiulizwa la Sinza Palestina, naomba nimjibu Mheshimiwa Said Kubenea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilishawahi kujibu hapa, Kituo cha Afya cha Sinza Palestina siyo Hospitali ya Wilaya. Katika jibu langu ambalo nililitoa siku ile nilitaka Halmashauri wahakikishe kwamba wanatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Nikajibu pia kwamba katika kituo cha afya na hii ni changamoto katika vituo vya afya vingi ambavyo viko mijini tunakosa jina hasa ambalo tungeweza kusema kwa sababu viko juu ya vituo vya afya

vya Kata za vijijini lakini pia havifikii hadhi ya Hospitali ya Wilaya. Ndiyo maana ukienda Sinza Palestina pale tumepeleka mpaka Madaktari Bingwa lakini bado hiyo haitoi mwanya kwamba tuseme ni Hospitali ya Wilaya. Kwa sababu Hospitali ya Wilaya inahitaji eneo la ukubwa usiopungua ekari 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishawaambia Halmashauri yake watenge eneo hilo ili tujenge Hospitali ya Wilaya kama ambavyo tunafanya kule Kivule kwa Mheshimiwa Waitara ili tuwe na hospitali za Wilaya kupunguza msongamano katika hospitali zingine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Mgumba, swali la nyongeza.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Morogoro mpaka sasa haina hospitali ya Wilaya na kwa kuwa Tarafa ya Ngerengere na mahali ambapo panajengwa hospitali ya Wilaya kuna umbali wa zaidi ya kilometa 105.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Ngerengere kuna miradi mitatu mikubwa ya Kitaifa ambayo ni *standard gauge* pamoja na ujenzi wa kiwanda cha sukari pamoja na Bwawa la Kidunda ambao unasababisha wingi mkubwa wa watu. Je, Serikali haioni umuhimu wa kukarabati Kituo cha Afya Ngerengere ili kiwe na hadhi ya kituo cha afya kuweze kuwa-*accommodate* watu hawa wote na kujenga Kituo kingine cha Afya katika Kata ya Mkulazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya kujibu naomba nitangulize maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo tumekuwa tunapata taabu pale ambapo pesa za maendeleo zinapelekwa hazifanyiwi kazi kwa wakati ni pamoja na kwa Mkurugenzi wa Halmashauri anayotoka Mheshimiwa. Kuna pesa zimepelekwa kwa ajili ya kujenga kituo cha afya lakini kasi yake ni mbovu sana. Naomba nichukue fursa hii kwanza kumuagiza Mkurugenzi ahakikishe kwamba pesa iliyopelekwa inatumika kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya ili wananchi waweze kupata huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha maeneo yale yote ambayo iko haja na kama ambavyo ametaja umbali na ni ukweli usiopingika kwamba Ngerengere ina umuhimu wake. Naomba nimhakikishie kwamba baada ya hili zoezi kukamilika na mimi nikapata fursa ya kwenda, tutashauriana namna nzuri ya kuweza kuhakikisha ukarabati unafanyika na huko.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Napenda kuipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale. Napenda niiulize Serikali, huduma ya *X-ray* kwa Wilaya ya Nyang'hwale ni shida sana. Kuna ajali mbalimbali ambazo zinatokea na kuifuata huduma ya *X-ray* karibu kilomita 110. Je Serikali ina mpango gani wa kuleta mashine ya *X-ray* katika Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamefanya vizuri kwenye suala zima la afya kwa maana ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati ni pamoja na kwa Mheshimiwa Amar. Naomba nimpongeze kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba *X-ray* zinakuwepo ndani ya vituo vyote vya afya na ndiyo maana katika maboresho ambayo yamefanyika hivi karibuni ni pamoja na kuongeza jengo la *X-ray.* Sasa kama *X-ray* zinakuwepo kwenye vituo vya afya sembuse hospitali ya wilaya! Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tukitoka hapa tuwasiliane tujue nini hasa ambacho kimetokea mpaka hospitali yake ya Wilaya ikose *X-ray. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali fupi.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wamekuwa wakishiriki huduma za afya kwa kujenga maboma. Kwenye Kata yangu ya Kimuri, wananchi wameweza kujenga vyumba zaidi ya 20 lakini vyumba hivi vimekaa zaidi ya miaka 10 Serikali haijaweza kukamilisha. Je, Mheshimiwa Waziri wako tayari kukamilisha hivyo vyumba ili wananchi waweze kupatiwa huduma bora ya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo Serikali tunaenda kujenga vituo vya afya pamoja na hospitali za Wilaya ni pamoja na Mkoa wa Kagera. Naamini Mheshimiwa Mbunge naye ni miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge

wanufaika katika Serikali ya Awamu ya Tano ambao wanaenda kupata huduma hii ambayo haikuwepo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la kukamilisha hivyo vyumba 20 ambavyo anavisema, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, wanasema kuona ni kusadiki. Ni vizuri pale ambapo tutapata nafasi ya kwenda kutazama ili tujue uhalisia na bajeti kiasi gani itahitajika kumalizia huo ujenzi ili nguvu ya wananchi isije ikapotea, kama Serikali tutakuwa tupo tayari.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 499

**Kada ya Maafisa Biashara Kutambulika kama Idara**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Tunapoelekea kujenga uchumi wa viwanda ni wazi kuwa fursa za kibiashara zinazojitokeza nyingi zitafanywa na wajasiriamali wadogo; hata hivyo muundo wa kazi kwa kada ya Maafisa Biashara katika Halmashauri zetu umefichwa ndani ya Idara ya Fedha, pamoja na kazi na uzito wa majukumu ya biashara siyo idara wala kitengo:-

Je, ni lini Wizara kwa kushirikiana na Utumishi itafanya kada hii kutambulika kwa uzito wake ili wanufaike na uwepo wa Maafisa Biashara kuliko ilivyo hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika muundo wa sasa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ulioidhinishwa mwaka 2011 wenye Idara 13 na Vitengo Sita, kada ya Maafisa Biashara ipo ndani ya Idara ya Fedha na Biashara. Napenda kulialifu Bunge lako Tukufu kuwa hivi sasa Serikali inaufanyia mapitio ya kina muundo huo kwa kuzingatia uzito wa kazi kwa kila kada ili kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Cosato David Chumi kwa kuwa maudhui ya swali lake yamechangia mawazo mazuri katika mapitio ya muundo wa Serikali za Mitaa yanayoendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali na pia kwa kukiri kwamba inaufanyia mapitio muundo na kwamba itazingatia mawazo ambayo nimeyatoa kutokana na swali langu, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, wakati huu ambapo tunaelekea uchumi wa viwanda, ni matarajio kwamba Maafisa Biashara tulionao watakuwa na wajibu zaidi ya wajibu walionao sasa ambao kimsingi umejielekeza zaidi katika kufanya kazi ya kutoa leseni na kukagua leseni. Maafisa hawa wengi wao ni watu ambao wana elimu zao, wamesoma mambo ya *international trade, international business* na kadhalika, kwa hiyo, tunakuwa kama tuna wa-*under utilize.* Je, lini mipango hiyo ya kukamilisha muundo itakamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali iko tayari wakati inaendelea kukamilisha suala hilo la muundo kuwa-*task* na kuwawezesha Maafisa Biashara ili waweze kuwasaidia wajasiriamali wetu kuibua miradi, kuwasaidia kuandika maandiko lakini pia kung'amua fursa mbalimbali za mikopo ya riba nafuu. Kwa mfano, kule kwetu Mafinga kuna

wafanyabiashara na wajasiriamali wa mazao ya misitu kama mbao, mirunda na nguzo na majirani zangu Njombe wanalima maparachichi. Je, Serikali wakati inaendelea kukamilisha muundo huo iko tayari kuwa-*task* na kuwawezesha ili wafanye shughuli hizo za kuibua miradi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nirejee katika swali langu la msingi nimemshukuru sana kwa mchango wake. Hata haya maswali yake mawili ya nyongeza bado ameendelea kuweka mchango mzuri wa mawazo ambao utakuja kusaidia sana Serikali. Yeye ana uzoefu mkubwa, amefanya kazi katika Serikali za Mitaa sehemu nyingi sana, kwa hiyo, uzoefu wake tutautumia. Hata baada ya leo hapa namkaribisha ofisini kwangu ili tujadiliane kwa kina zaidi haya masuala ya Serikali za Mitaa kwa sababu wote tuna uzoefu nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wajibu wa Maafisa Biashara, muundo utakapokamilika wataongezewa wajibu zaidi, kwa sababu sasa kama tunawatoa kwenye ile Idara ya Fedha tunawapeleka kwenye Idara nyingine ambavyo sipendi kuitaja kwa sababu haijawa rasmi watashirikiana huko na Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wachumi katika kutekeleza yale ambayo Mheshimiwa Mbunge anayependekeza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kutokana na mwamko uliopo wa wananchi kujiunga na vikundi vya ujasiriamali pamoja na

*VICOBA* lakini wananchi wamekabiliwa na kutokuwa na uwezo wa uzalishaji. Tatizo hili linachangiwa na kutokuwepo na Maafisa Biashara wa kutosha katika Halmashauri zetu na kuwajengea uwezo wananchi. Halmashauri zote nchini zina Afisa Biashara mmoja au wawili au hakuna kabisa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaajiri Maafisa Biashara wa kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema katika mazingira ya sasa kuna vikundi vingi vya uzalishaji mali, kuna *VICOBA* na shughuli nyingi za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Kalemani na timu yake kueneza umeme vijijini na kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Profesa Mbarawa na timu yake kujenga barabara na sisi kupitia *TARURA* kujenga barabara za vijijini, fursa nyingi sana zinajitokeza. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa sana iliyoko mbele yetu ambayo tunahitaji kuifanya kupitia kada hizi za Afisa Biashara, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wachumi. Serikali itahakikisha kwamba wanapatikana wa kutosha ili kusudi wananchi wahudumiwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ukataji wa leseni unaenda sambamba na uwasilishaji wa *tax clearence* katika Halmashauri zetu na uwasilishaji wa *tax clearance*

unaamaanisha kwamba watu wamelipa kodi, kwa maana hiyo watu wanalazimika kulipa kodi kabla hata ya kufanya biashara. Je, hatuoni kwamba ni muhimu kuondoa kigezo cha *tax clearance* katika baadhi ya biashara ili watu waweze kukata leseni na kuanza biashara kabla ya kulipa kodi na kabla ya biashara zenyewe kuanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Fedha sijui yuko hapa ama Naibu Waziri wa Fedha na sijui kama wamesikia swali. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake linalenga kujaribu kutetea wafanyabiashara wale wanaoanza na utetezi wa aina hiyo siyo mbaya, ni mzuri. Hata hivyo, kwa sababu kuna kanuni, sheria na taratibu ambazo zimewekwa, nalichukulia swali lake kama mchango wa maoni ambao unahitaji kufanyiwa kazi baadaye lakini kwa leo hatuwezi kutoa tamko kwamba sasa tunafuta taratibu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuhusu swali hili nadhani kama watu walisikiliza hotuba ya Waziri alilizungumzia jambo hili. Kwa hiyo, nadhani tusubiri tuone *Finance Bill* inasemaje, tuipitie. Nadhani alilizungumzia jambo hili na kwamba na wao wameliona kama changamoto na wanalifanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Zainab Katimba, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa jitihada za kutoa mitaji kwa vijana na wanawake inabidi ziende sambamba na kuwajengea uwezo wa

kuanzisha na kuendeleza biashara. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatumia hawa Maafisa Biashara katika kuwajengea uwezo vijana wanaokuwa katika vikundi ambao wananufaika na asilimia 10 inayotengwa kutoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kwa dhati kabisa nimshukuru na kumsifu sana Mheshimiwa Zainab Katimba kwa sababu yeye amekuwa anashughulikia sana sana maslahi ya vijana katika Bunge hili Tukufu. Aliwahi kuleta mpaka mapendekezo ya hoja kutaka kutetea vijana wanaomaliza shule ili kusudi waajiriwe bila kuwa na *experience*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie kwamba vijana katika nchi hii wana idara nyingi sana za kuweza kuwasaidia mawazo ya kujikwamua kutoka pale walipo kwenda mbele. Katika Halmashauri kuna Idara ya Vijana, Idara ya Maendeleo ya Jamii na Idara ya Mipango sasa Maafisa Biashara tunawongezea sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nitumie nafasi hii kuwaomba vijana wa nchi hii ambao hata fursa ambayo ziko katika Halmashauri hawazitumii ipasavyo, ukienda katika Halmashauri unakuta maombi ya vijana yako asilimia 10 ya maombi yote yaliyowasilishwa. Kwa kweli, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tujitahidi kuwaelimisha na kuwaomba vijana wajitokeze na wajiunge katika vikundi na watumie fursa zilizopo kwa ajili ya kujiendeleza na Serikali tuko macho katika kuangalia suala hilo linatekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela, swali la nyongeza.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na Serikali kuendelea kutenga maeneo ya kibiashara kwa ajili ya wajasiriamali wadogo, lakini bado kumekuwa na changamoto kubwa kwa wajasiriamali hawa wadogo hususani katika Manispaa ya Mpanda Mjini kwamba wamepelekwa kwenye maeneo ambayo miundombinu ya kibiashara pamoja masoko imekuwa na changamoto kubwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wajasiriamali hawa katika Manispaa ya Mpanda Mjini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka juzi Serikali imetoa maelekezo kila Halmashari, Wilaya na mkoa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji. Uwekezaji ni kuanzia uwekezaji mdogo, wa kati na mkubwa hususani maeneo ya viwanda, viwanda vidogo, viwanda vya kati na vikubwa na yawepo maeneo maalum kwa ajili ya biashara katika kila mji na kila Halmashauri. Kwa hiyo, hayo ni maelekezo ambayo yanakwenda kuboresha maeneo yetu ya Miji, Halmashauri na minada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hayo maelekezo ya Serikali yatakapokamilika kutekelezwa vizuri, miundombinu ni sehemu ya mahitaji kwenye maeneo hayo mapya. Kwa hiyo, tunazidi kusisitiza kila halmashauri inapotenga eneo jipya lazima liambatane na miundombinu inayohitajika, ikiwemo umeme, maji na vyoo. Kwa hiyo, masuala yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyazungumza, kama ni

Mpanda basi tutafuatilia tuhakikishe kwamba hiyo miundombinu inayokosekana inakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 500

**Kukarabati Majengo ya Stesheni za Reli ya Kati**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Stesheni Kuu, vituo vidogo vidogo na maeneo yanayozunguka Stesheni za reli ya kati vimechakaa sana:-

Je, Serikali haioni haja ya kukarabati majengo ya Stesheni za reli ya kati na kuweka miundombinu ya maji safi na maji taka katika majengo hayo na maeneo yanayozunguka stesheni hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASHTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* lina jumla ya stesheni 124 katika mtandao wake wa reli hapa nchini. Aidha, shirika lilishaanza ukarabati wa stesheni za treni ambao pamoja na mambo mengine umezingatia uboreshaji wa mifumo ya maji safi na maji taka pamoja na sehemu za kukaa abiria wakati wa mvua kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, stesheni zilizokwisha kukarabatiwa ni pamoja na Kigoma, Kaliua, Pugu, Malindi na Mwanza ambapo ukarabati bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika linatambua changamoto ya ukosefu wa baadhi ya huduma katika stesheni zilizobakia za reli kutokana na kuwa na miundombinu chakavu na hivyo kuweka mpango mkakati wa kukarabati na kuboresha stesheni hizo hatua kwa hatua kadri hali ya kifedha itakavyokuwa inaruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pia nashukuru kwa majibu hayo yaliyotolewa na Serikali na kwa kuwa bado stesheni zetu nyingi hasa ikiwemo hii ya Makao Makuu bado hazina sura ya kuvutia na kwa kuwa huduma za vyoo na maji ni muhimu sana kwa afya, majibu ya Serikali yameeleza kwamba itategemea upatikanaji na vyanzo vya ndani, ambavyo vinaweza vipatikane au visipatikane au vitengwe au visitengwe. Je, ni kwa nini Serikali isitenge ikahaulisha kwenye mafungu mengine kufanyia matengenezo huduma hizi muhimu kwa afya ya wananchi wengi hasa wenye uwezo mdogo ambao wanatumia reli hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa watoaji wa huduma wengi kwenye reli hii ni wajasiriamali wadogo akinababa lishe, akinamama lishe na vijana. Kwa nini Serikali isiwafanyie utaratibu wa kujenga *sheds* au miavuli iliyopangika kwa utaratibu unaolekeweka wakafanya shughuli zao kuliko kutawanya masufuria, majungu, majiko, kuni *along the railway lane?* Na kwa nini Serikali...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, maswali ni mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO – (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hali ya Shirika la Reli Tanzania halijaimarika sana; lakini tukumbuke tu kwamba Shirika la Reli nalo linafanya biashara na linao wajibu na jukumu la kuhudumia wateja wake. Pale watakapoona kwamba wameshindwa tutataarifiana ndani ya Wizara halafu tutajua namna ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili, ni kweli kwamba wajasiriamali wapo wengi kwenye *station* zetu mbalimbali hapa nchini na wamekuwa wakifanya shughuli pamoja na Shirika letu la Reli. Ni jukumu sasa la Shirika la Reli wakae na hao wajasiriamali waweze kuwatengenezea mazingira wezeshi ya kufanya shughuli zao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya swali la nyongeza.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Watumishi wanaofanya kazi kwenye njia ya reli kwenye vituo vidogo *(gangs)* wanafanya kazi ngumu, kwenye mazingira magumu, lakini wamekuwa hawalipwi fedha zao kwa wakati. Kwanza ni vibarua lakini kuna wakati wanakaa wanapewa baada ya miezi miwili mitatu, wanaishi katika hali ngumu sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanalipwa fedha zao kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa sababu ni mdau mkubwa sana wa reli, amekuwa akiitumia miaka mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *gangs* zetu nyingi sana zimekuwa chakavu na nyingine tumezifunga

kutokana na uchakavu huo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Shirika la Reli lipo kwenye mchakato wa kuanza kuzirekebisha *gangs* zote nchini, kwa sababu kutokuwepo kwa *gangs* kumesababisha hata hujuma mbalimbali kwenye reli yetu na kusababisha upotevu wa mali na wakati mwingine hata maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutahakikisha kwanza tunazirekebisha *gangs* zetu, lakini tumeomba kibali kwa ajili ya kufanya ajira nyingine zaidi kwa sababu hata waliokuwepo wameshafikia umri wa kustaafu lakini tumeamua kuwa-*hold*. Tutakapofikia hatua hiyo hali itabadilika na utaona kabisa kwamba wale nao wataanza kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Nchemba, swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. NCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa *station* hizo zina Vituo vya Polisi na kwa kuwa kwa muda mrefu sana Vituo hivyo vya Polisi havija pata msaada wa kukarabatiwa, pamoja na nyumba zao ni chakavu, mbovu, hazifai. Je Serikali iko tayari sasa kutenga fedha rasmi kwa ajili ya ukarabati wa Vituo hivyo vya Polisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO – (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye program ambayo imewekwa na Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* pamoja na ukarabati wa *station* watakarabati na Vituo vya Polisi ambavyo vipo kwenye *station* mbalimbali. Kwa hiyo tunamwomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati mchakato huo utakapoanza hivi karibuni hivyo vituo navyo vitakarabatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na juhudi za Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutekeleza Irani ya Chama cha Mapinduzi, kujenga reli ya kisasa ya *Standard Gauge* ambayo naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi; matatizo ya vituo vidogo vidogo pia yanawapata wakazi wa Dar es Salaam katika Treni yao ya *station* kwenda Pugu. Hakuna vituo vidogo vya kushushia abiria katika treni hiyo inayotoka *station* pale mjini kwenda Pugu. Treni inasimama tu na watu wanashuka shuka tu. Je Serikali ina mpango gani wa kuboresha vituo vya treni hiyo ambayo ni muhimu sana kwa wakazi wa Pugu, Ukonga, Kiwalani, Kipawa, Yombo na Vituka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO – (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa jinsi anavyofuatilia sana ile reli ambayo imebatizwa jina la Reli ya Mwakyembe. Ni reli muhimu sana kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na imekuwa ikitoa huduma mbalimbali za kusaidia usafiri katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vilivyopangwa kwa ajili ya kuhudumia reli hiyo ambayo inaitwa kwa jina la Mwakyembe ni vile ambavyo vilikuwa vinatumika kwenye reli ile ya toka mwanzo; na hatuna mpango mpaka sasa hivi wa kubadilisha. Nawaomba Watanzania na wakazi hasa wa Dar es Salaam wasishuke kama treni haijasimama, ni lazima waendelee kuheshimu kwamba treni ina vituo vyake maalum na ikisimama ndio mtu ashuke au kupanda, wasipandie njiani kwa sababu wanaweza kupata ajali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Vedasto Edga Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 501

**Usikivu Hafifu wa TBC Maeneo ya Vijijini.**

**MHE. VEDASTO EDGA NGOMBALE (KILWA KASKAZINI)** aliuliza:-

Kupata habari ni moja ya haki za Kiraia, *TBC* ni chombo pekee cha habari kwa sasa kinachowafikia wananchi wengi hususan wale wanaoishi vijijini lakini kwa muda mrefu sasa chombo hicho hakisikiki vizuri katika maeneo mengi ya vijijini vya Jimbo la Kilwa Kaskazini na Wilaya ya Kilwa kwa ujumla.

Je, ni tatizo gani linalosababisha chombo hiki kisisikike vizuri katika maeneo mengi ya vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edga Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kuchukua hatua mahsusi za kuboresha usikivu wa Redio katika Mikoa ya Lindi pamoja na Mtwara, ikiwemo Wilaya ya Kilwa kama ifuatavyo:-

(a) Mitambo ya kurushia matangazo iliyoko Nachingwea ya *TBC* Taifa imeongezewa nguvu kutoka *watt* 250 hadi *watt* 1,000 na ile ya *TBC FM* toka *watt* 150 hadi *watt* 1,000. Matokeo yake ni usikivu bora wa redio maeneo mengi ya Nachingwea, Ruangwa na sehemu za Wilaya ya Masasi.

(b) Mitambo miwili ya kurushia matangazo ya *TBC* Taifa na *TBC FM* imejengwa Mtwara, kila mmoja una ukubwa wa *watt* 1,000 na kuwezesha matangazo ya redio kuwafikia wananchi Mtwara Vijijini, Tandahimba pamoja na Lindi Vijijini.

(c) Hatua ya tatu ni ndani ya mwaka wa fedha 2018/2019 tuna mradi wa kujenga Mtambo mpya wa *FM* wa kurusha matangazo eneo la Nangurukuru ambao utaimarisha usikivu wa redio maeneo ya milima yaliyobaki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedasto Ngombale swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza *community* redio ya *Mashujaa FM* kwa kufanya *coverage* kwa niaba ya *TBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Serikali ilitenga hiyo bajeti ya kujenga mtambo Nangurukuru, mwaka 2017/2018 na hii 2018/2019 imerudia kuwa inaendelea kutenga bajeti bila ya utekelezaji. Sasa nini *commitment* ya Serikali katika bajeti ya mwaka huu kwa sababu inaonekana kana kwamba Serikali haina nia thabiti ya kujenga mtambo huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa *TBC* ndio chombo cha Taifa na kina jukumu la kutoa mawasiliano kwa wananchi, kutokana na kusua sua kwake Mheshimiwa Waziri haoni kwamba wanawakosesha haki wananchi wa Kilwa kupata habari? Lakini pia...

**NAIBU SPIKA:** Mawili tayari Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ameonesha wasiwasi kwamba *TBC* inasuasua katika utekelezaji wa usikivu hususan katika Wilaya yake ya Kilwa.

Kwanza napenda kutumia nafasi hii kumtoa hofu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kwanza, wote tunafahamu kwamba katika bajeti ya fedha ya mwaka WA 2017/2018 Serikali ilitenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuboresha usikivu wa *TBC* na fedha hiyo ilishatolewa yote. Katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga bajeti ya shilingi bilioni tano. Kwa hiyo tuna imani kabisa fedha hiyo itatolewa yote kwa sababu imekuwa ni mpango wa Serikali na tumeona kabisa Serikali ina *commitment* na ndiyo maana katika fedha zote ambazo zinatengwa zimeendelea kutolewa kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, kwamba *TBC* kusuasua kwake kunawakosesha haki wananchi, nimtoe hofu kama ambavyo tumejibu katika jibu letu la msingi, kwamba katika mwaka huu wa fedha wa 2018/2019 Serikali kupita shirika lake la *TBC* imejipanga kujenga mnara mpya wa kurushia matangazo yake katika eneo la Nangurukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaamini kabisa na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mimi kama Naibu Waziri pamoja na Waziri wangu tutawasimamia katika mwaka huu wa fedha kuhakikisha kwamba mtambo huo unajengwa, ili basi wananchi wa Kilwa waweze kupata haki yao ya kuweza kupata habari, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nitoe shukurani kwa Wizara hii kwa sababu wametujengea mtambo katika eneo letu la Kwemashai kule Lushoto; lakini bado usikivu haupo vizuri. Sasa, je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba usikivu wa *TBC* katika Wilaya ya Lushoto na leo wenyewe wapo hapa wamekuja kufuatilia jambo hili utakuwa na usikivu unaoeleweka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa sababu yeye amekuwa ni mdau mkubwa wa *TBC* ndani ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kama ambavyo ametoa pongezi na mimi kwa niaba ya Serikali napenda kupokea pongezi hizo, kwamba *TBC* sasa hivi tumekwisha kuweza kujenga Mtambo katika Wilaya yake ya Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo ipo katika Wilaya hiyo ya Lushoto ambayo inasababisha usikivu kutokuwa mzuri ni kwamba mitambo hii inapofungwa lazima kuwe kuna muda kidogo wa kuweza kufanyia maboresho. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuweza kumhakikishia Mheshimiwa Shangazi, pamoja na wananchi wote wa Wilaya ya Lushoto ambao wapo ndani ya Bunge hili, kwamba ndani ya miezi miwili nilishaongea na Mkurugenzi wa *TBC* ameniahidi kwamba atatuma timu yake ya wataalam kwenda kufanya maboresho katika mtambo huo ili basi usikivu wa *TBC* uwe mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Swali kama hili ambalo Mheshimiwa Ngombale leo ameuliza, nililiuliza mimi 2016 na majibu yalikuwa haya haya. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkoa wa Lindi usikivu wa *TBC* ni tatizo sana, naomba *commitment* ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama alivyotoa wakati anajibu kwa Mheshimiwa Ngombale; kwamba katika mwaka huu wa fedha huo mnara aliosema utajengwa ili Watanzania wanaomsikia wajue kwamba Serikali imeji-*commit* ndani ya Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**WAZIRI WA HABARI UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa ambayo ameyatoa kwa maswali aliyoulizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Bobali kwamba, kwanza si sahihi kusema kwamba eti majibu tuliyotoa sasa ndio majibu tuliyotoa kipindi kilichopita miaka miwili iliyopita wakati kuna miradi tayari tumeitekeleza mwaka huu na mwaka jana. Ni kichekesho, sasa sisi tumekuwa waganga wa kienyeji kwamba tumetekeleza hayo mambo mwaka huu..

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge awe na imani na Serikali yetu, kwamba tumehakikisha kwamba katika mwaka 2018/2019 mradi wa kujenga mtambo wa *FM* kurusha matangazo eneo la Nangurukuru utatekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mkoa wa Katavi usikivu wa *TBC* sio mzuri kabisa na baadhi ya maeneo hawasikii matangazo ya aina yoyote na hutumia matangazo ya nchi jirani. Je, ni lini Serikali italeta mtambo kwenye Mkoa wa Katavi ili wananchi waweze kupata huduma ya *TBC*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 ipo mikoa mitano ambayo ipo kwenye bajeti. Mikoa hiyo ni mikoa mipya ukiwemo Mkoa wa

Songwe, Mkoa wa Simiyu, Mkoa wa Katavi, Zanzibar pamoja na Mkoa wa Njombe. Kwa hiyo nichukue nafasi hii kuweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, Mkoa wa Katavi upo kwenye mpango na tunamhakikishia kwamba usikivu wa TBC katika Mkoa wake utaboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mmesimama wengi hapa, Mheshimiwa Devota Minja, swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Sote tunafahamu kuwa *TBC* ni chombo cha umma na kinaendeshwa kwa kodi za Watanzania. Jana wakati tunapiga Kura ya kupitisha bajeti *TBC* ilikuwa live bila chenga; lakini kipindi chote tunadadavua kuhusu bajeti *TBC* haikuwa *live* kuwaonesha wananchi ni kitu gani tunajadili. Hivi kulikuwa kuna haja gani ya kuonesha ndiyo au hapana kama siyo Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inataka kuwahadaa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Sina uhakika hilo swali lako linahusiana na swali la msingi kwa sababu ni swali la msingi linahusu kusikika kwa *TBC* ama kutazamwa na wananchi sehemu nyingine. Kwa hiyo, hilo swali lako Mheshimiwa halina uhusiano na swali la msingi. Mheshimiwa Deo Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ludewa kijiografia ni tambarare, milima na mabonde na kwa maeneo mengi inayosikika inasikika Redio Malawi. Je, ni lini *TBC* itasikika maeneo ya Ludewa yote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo

nimeshajibu kwamba, katika mwaka wa fedha 2018/2019 *TBC* imetengewa bajeti ya shilingi bilioni tano. Kati ya mikoa ambayo itashughulikiwa ni Mkoa wa Njombe. Kwa sababu natambua kabisa kwamba Wilaya ya Ludewa ipo ndani ya Mkoa wa Njombe, kwa hiyo, ni hakika kabisa kwamba *TBC* ndani ya mwaka huu wa fedha itaweza kusikika na maboresho makubwa yatafanyika katika Wilaya hiyo ya Ludewa pamoja na Mkoa mzima wa Njombe.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mheshimiwa Cecylia Daniel Pareso Mbunge wa Viti maalum sasa aulize swali lake.

Na. 502

**International Great Lakes Woman Research and Documentation Centre**

**MHE. CECILIA D. PARESO** aliuliza:-

Serikali ilihusika kikamilifu katika uanzishwaji wa kituo kijulikanacho kama *International Graet Lakes Woman Research Centre* ambapo kwa Tanzania kituo hicho kuliazimiwa kiwe Tengeru Arusha:-

(a) Je, mpaka sasa utekelezaji wake umefikia wapi?

(b) Je, ni mafanikio gani yamepatikana tangu kituo hicho kianzishwe?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha *Great Lake Woman Recherch and Documentation Centre* kilianzishwa mwaka 2009 ikiwa ni utekelezaji wa maazimio kikao cha Mawaziri, wanaosimamia masuala ya wanawake kutoka nchi za Maziwa Makuu kilichofanyika mwezi Julai, 2008 Kinshasa, Jamuhuri ya Demokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini kituo hicho kilianzishwa chini ya Taasisi ya Maendeleo ya Jamii, Tengeru kwa malengo ya kufanya utafiti kuhusu masuala ya maendeleo ya jinsia na wanawake hapa nchini, kuhifadhi matokeo ya tafiti hizo ili kuwasaidia watunga sera na wafanya maamuzi kukusanya taarifa na takwimu mbalimbali zinazohusiana na jinsia na wanawake pamoja na kusambaza taarifa hizo kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizofikiwa katika kuanzisha Kituo hicho, ni pamoja na kutenga eneo maalum ndani ya taasisi linalotumika kwa ajili ya kituo; kukipatia Kituo hicho rasilimali watu ikiwemo Mratibu wa Kituo pamoja na Mkutubi kwa ajili ya kuendesha na kusimamia shughuli za kituo; Kukipatia kituo vifaa ikiwemo *computer* ishirini na nne, mashine ya *fax* na simu; kuanzisha tovuti ya kituo inayopatikana kwa anuani ya *www.wrdc. or.tz* kwa ajili ya kuwafikia watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuanzishwa kwa kituo hicho baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kutoa mafunzo ya ujasiriamali, kwa wanawake na wanaume ili kuwajengea uwezo wa kuendesha shughuli zao na kujiongezea kipato kwa ufanisi na hivyo kupunguza umasikini kwenye jamii. Aidha, chuo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi mia mbili wa shule za sekondari ili kuwajengea uelewa wa masuala ya ukatili wa jinsia na madhara yake katika kujenga uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kituo kimewahudumia zaidi ya watu mia tatu ishirini kati ya hao wanawake mia mbili thelathini na moja na wanaume sabini na tisa; na kuwawezesha kupata taarifa walizozihitaji zenye

kuelimisha kuhusiana na masuala ya haki za umiliki wa ardhi kwa wanawake, ukatili wa kijinsia na elimu ya ujasiriamali kupitia tovuti na machapisho mbalimbali yaliyopo kwenye Kituo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa malengo ya kuanzishwa kwa kituo hicho ilikuwa ni maamuzi ya Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya jinsia na wanawake; na kwa kuwa malengo haya yalijikita katika kuhakikisha kunakuwa na kituo ambacho kitasaidia uwezeshwaji wa ufanyaji wa tafiti na kuhifadhi machapisho hayo ya utafiti na kuwashauri watunga sera kuhusiana na masuala mazima ya maendeleo ya wanawake na jinsia; ni ukweli kwamba pamoja na kuzindua kituo hiki lakini Serikali haijweka msisitizo wa kukiwezesha kituo hiki kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Je, Serikali sasa iko tayari kufufua mchakato huu wa kukianzisha kituo hiki ili kiweze kutimiza malengo ya uanzishwaji wa kituo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutenga eneo kama ambavyo wameeleza katika Chuo cha Tengeru ni jambo moja na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu na rasilimali fedha ni jambo lingine. Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha inakipatia fedha kituo hiki ili malengo ya uanzishwaji wake yaweze kutimia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Paresso amesema kwamba je, Serikali ina mkakati gani wa kukifufua. Niseme tu kwamba kituo hiki kipo na nilipata fursa ya kutembelea Chuo cha Tengeru na

kukitembelea hiki kituo. Kipo na kinafanya kazi. Kwa hiyo kaika hoja kusema kwamba tunahitaji kukifufua hili halipo kwa sababu ni kituo ambacho kinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la kuongeza rasilimali watu na rasilimali fedha kituo hiki pamoja na kwamba lilikuwa ni azimio, sisi kama Serikali kupitia Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii tunaendelea kukihudumia kituo hiki kuhakikisha kwamba kinafanya kazi na kadri rasilimaliwatu itakapokuwa inaongezeka na sisi tutaongeza watumishi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeenda mbali zaidi; kwa sababu ya majukumu ya kituo hiki katika kutoa elimu na uelewa katika masuala ya jinsia tumeendelea kuwasiliana na taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu na taasisi mbalimbali ambazo zinafanya tafiti katika masuala ya jinsia ili nao watusaidie kutupatia yale machapisho yao na kuyahifadhi katika maktaba zetu hizi kwa lengo la kupanua wigo kwa kupata machapisho mbalimbali yanayohusiana na masuala ya jinsia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 503

**Kuboresha Sekta ya Utalii**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Sekta ya Utalii imekuwa ikitoa ajira kwa vijana wetu wa Visiwani na Tanzania Bara; kutetereka kwa sekta hii kumesababisha kupungua kwa ajira kwa kiasi kikubwa na vijana kurudi mitaani;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha na kuboresha sekta hii ili ajira zipatikane kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta muhimu katika uchumi wa Taifa ambapo sekta hii huchangia zaidi ya asilimia 17 ya Pato la Taifa *(GDP)* na asilimia 25 ya fedha za kigeni nchini. Sekta hii inatoa ajira nyingi za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja hapa nchini ambapo kwa sasa sekta ya utalii huchangia ajira takriban 1,500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mkubwa wa sekta ya utalii katika kuchangia ajira nchini, Wizara inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuongeza fursa za ajira ikihusisha:-

(i) Kupanua wigo wa mazao ya utalii ili kuongeza fursa za ajira kama vile; utalii wa mikutano, utalii wa fukwe, utalii wa matamasha mfano urithi *festival,* utalii wa miamba *(geo-tourism),* utalii wa meli, utalii wa reli, mfano *TAZARA* na Tanga *Line,* utalii wa michezo, utalii wa matibabu na kadhalika.

(ii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Utalii. Katika kutekeleza hili, Wizara imekamilisha zoezi la kubaini maeneo ya fukwe katika mwambao wa bahari ya Hindi kwa ajili ya uwekezaji wa shughuli za utalii.

(iii) Wizara inaendelea kuhamasisha wananchi kuanzisha miradi ya utalii wa utamaduni *(Cultural Tourism Programme)* ambapo mpaka sasa miradi 66 imeshaanzishwa katika mikoa mbalimbali nchini.

(iv) Wizara kupitia Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii hutoa mafunzo ya kozi za utalii na ukarimu katika ngazi ya astashshada na stashahada. Kozi hizo zimesaidia kupata

wahitimu wenye ujuzi unaohitajika katika soko la ajira za sekta ya utalii.

(v) Kuimarisha miundombinu ya usafiri wa anga, nchi kavu na baharini, kuanzisha *channel* na studio mahsusi kwa ajili ya kutangaza utalii, kuhamasisha wawekezaji kwenye maeneo ya utalii na kuandaa na kutangaza utambulisho wa Taifa *(destination branding).*

(vi) Aidha, Sheria ya Utalii ya mwaka 2008, kifungu cha 58(2), imetenga shughuli mahsusi za biashara ya utalii kwa ajili ya Watanzania. Vile vile, Wizara imepunguza ada ya leseni za biashara ya utalii kwa lengo la kuwawezesha Watanzania wengi kushiriki kufanya shughuli za utalii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Msabaha, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Naibu Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, pamoja na Serikali kutoa elimu katika sekta hii ya vyuo vya utalii, lakini wamekuwa wakichukua wanafunzi ambao wamefeli au wanapata *division four* na kutofanya vizuri katika vyuo vingi na kusababisha hoteli nyingi za kitalii kuajiri wafanyakazi kutoka nje. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha vyuo vya utalii ili kuhakikisha wanachukua wale wanafunzi ambao wanafanya vizuri ili sekta hii iweze kufanya vizuri katika anga za kimataifa na hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wenzetu Kenya, kwa mfano unatokea London unafika *Airport* ya Kenya, watalii wengi wanashuka sana Kenya na unaona ni namna gani wenzetu wamejitangaza katika sekta hii ya utalii na kupunguza tozo katika suala la utalii. Nauliza Serikali, je, haini sasa kuna umuhimu wa kupunguza kodi katika sekta hizi za utalii ili tuweze kufanya vizuri na kuingiza Pato la Taifa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba kumekuwa na upungufu wa wataalam katika Sekta hii ya Utalii na ndiyo maana kwa kuliona hilo, Serikali imechukua hatua ya kuhakikisha kwamba kwanza tunakiimarisha chuo chetu cha utalii ili kiweze kutoa mafunzo. Kwa hivi sasa kilikuwa kinatoa mafunzo katika ngazi ya stashahada na astashahada, lakini kuanzia mwaka 2019 kwa ushirikiano pamoja na chuo cha Canada *(Vancouver)* tumeamua kwamba sasa tuanzishe *programme* ya kutoa *degree, degree* hizo zitasaidia kuandaa wataalam mbalimbali ambao watashiriki katika sekta ya utalii. Baadhi ya *degree* ambazo tunategemea kuzianza ni hizi zifuatazo:-

(a) Digrii ya ukarimu *(degree in hospitality operations) ;*

(b) Digrii ya Utalii *(degree in travel and tourism management)* na

(c) Digrii ya Utaratibu wa Matukio *(degree in events management)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika hizi *degree* tatu zitakapoanza ni imani yetu kwamba tutakuwa tunaweza kupata wataalam wale ambao sasa watakuwa wanatoka hapa hapa nchini na kuweza kuhudumia vizuri sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo pia tunawahamasisha wawekezaji katika vyuo vingine vya binafsi waweze kuwekeza katika eneo hili kwa sababu sasa hivi mahitaji bado ni makubwa na wataalam bado ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kwamba tunachukua wale waliofeli, si kweli. Kwa mujibu wa taratibu zilizopo katika nchi hii, watu wote waliomaliza hata kama yuko *division four*

kama ana 'D' nne na kuendelea anaruhusiwa kujifunza na ngazi ya cheti (astashahada) na akifaulu anaendelea katika ngazi ya stashahada. Kwa hiyo, nadhani kwamba mkakati huu bado hatuchukui wale ambao ni *failure,* tunachukua wale ambao wana sifa za kujiunga na hivi vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili kuhusu kupunguza kodi katika huduma mbalimbali za utalii; ni azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kwamba kodi hizi zinapunguzwa ili wawekezaji na watu mbalimbali waweze kushiriki katika hizi shughuli za utalii; na mmesikiliza katika hatua mbalimbali ambazo tumechukua. Hivi sasa bado tunaendelea kutazama ni aina gani za kodi ambazo zinaweza zikapunguzwa zaidi ili kusudi hii sekta iweze kuimarika zaidi nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Mtuka, subiri kwanza Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimependa niongeze majibu ya nyongeza kutokana na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada tunazofanya za kuongeza kozi ambazo zinatolewa kwenye Chuo chetu cha Utalii lakini pia tunatambua kwamba sekta ya utalii pamoja na kwamba inaajiri watu zaidi ya 1,500,000 Chuo chetu cha Utalii toka kimeanza kimetoa wahitimu wasiozidi 5,000. Kwa maana hiyo wanaofanya kazi kwenye hoteli si lazima kwamba wanatoka kwenye chuo chetu cha utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hilo na kwa kutambua kwamba kuna wadau wengine ambao wanatoa taaluma ambazo zinatumika kutoa huduma kwenye sekta ya utalii kama *VETA* na vyuo vingine ambavyo vimesajiliwa na *NACTE,* tumeona tuanzishe mtihani wa Kitaifa ambao utaweka *standard* pamoja zote kwa usawa ili kila anayehitimu atoke kokote kule anakotoka afanye huo

mtihani, aingie katika vigezo ambavyo vitakuwa vinatambulika kitaifa na sasa ndiyo aende kuajiriwa kwenye sekta ya utalii. Kwa sababu tunaamini, ili tuweze kupata watalii wengi, ni lazima tuongeze ubora wa huduma tunazotoa ili watalii wapate *experience* nzuri na wanapoenda kule kwao warudi tena kutalii lakini pia waseme maneno mazuri kwa watu wengine katika *cycles of influence* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo pamoja na jitihada hizo, tumetunga kanuni za kufanya *certification* ya *professionals* wanaotaka kuajiriwa kwenye sekta ya utalii, lakini pia tunaanzisha mafunzo ya Uanagenzi katika hoteli na maeneo yote ya utalii ili ku-*boost* kidogo *quality* ya watoa huduma kwenye Sekta ya Utalii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Daniel Mtuka, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kw akunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Manyoni hususan Jimbo la Manyoni Mashariki tunavyo vivutio vingi sana vya utalii. Kwa mfano, tunazo kumbukumbu ya kituo kikubwa cha msafara wa watumwa wa njia ya kati kuanzia Ujiji, Unyanyembe kwenda Bagamoyo, lakini pia tunayo kumbukumbu ya ngome kuu ya Wajerumani iliyotumika kupambana na Mtemi Mkwawa wa huko Uheheni; lakini pia tuna jiwe la picha ya Bikira Maria kule Iseke. Je, Serikali iko tayari kusaidia kutangaza vivutio hivi ili kuinua kiwango cha ajira? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, mimi mwenyewe juzi Jumamosi nilikuwa kule Wilaya ya Manyoni na nimetembelea katika maeneo yote aliyoyataja na kuona utajiri mkubwa ambao Wilaya ya Manyoni inao hasa katika haya maeneo ambayo ameyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ambazo tunategemea kuchukua kama Wizara ni kwamba tutakwenda tutatangaza sasa vivutio vyote vile pamoja na historia nzuri ambayo ipo pale. Kuna jiwe moja ambali linajulikana kama jiwe la mjusi lakini zaidi ya hapo tumefika sehemu ambayo tunaita ndipo kitovu cha nchi hii yaani katikati ya Tanzania. Kuna maeneo mengi sana yenye vivutio vizuri sana kule Manyoni ambayo tutayatangaza sanjari na hatua ambazo tunazichukua katika kutangaza utalii katika maeneo yote nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Risala Kabongo, swali la nyongeza.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa wamiliki wengi wa hoteli za kitalii wanatumia wanafunzi waliopo kwenye mafunzo ya vitendo kufanya kazi za kuhudumia watalii na baada ya muda huo hawaajiriwi. Mchezo huu unasababisha ukosefu wa ajira kwa wahitimu kwa muda mrefu na kuikosesha Serikali mapato. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua taizo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza yeye mwenyewe ni mhifadhi mzuri sana, kwa hiyo nampongeza sana kwa kuwa mhifadhi mzuri na naamini atatumia taaluma yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwamba, hoteli nyingi zimekuwa kweli zinawapokea vijana wanaotoka katika vyuo mbalimbali kwa ajili ya kupata *field* yaani kupata uzoefu ili waweze kwenda kuajirika katika maeneo mbalimbali. Hii ni hatua nzuri. Kwa hiyo, nafikiri hii ni ya kui-*encourage* zaidi ili kusudi hoteli nyingi zipokee hao vijana wetu, wafundishwe namna ya kufanya kazi kwa vitendo ili wanapoajiriwa pale waweze kutumia taaluma zao vizuri na waweze kufanya kazi ya kutoa huduma ile ambayo inastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kuhusu ajira, ni kwamba tutaendelea kuhamasisha wawekezaji na hoteli mbalimbali ili ziweze kuwapokea vijana wetu ambao wamehitimu katika vyuo mbalimbali ili waweze kuajiriwa na waweze kutoa ile huduma nzuri. Pamoja na yale majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameshayatoa, basi jitihada hizi tunaamini kabisa kwamba zitasaidia sana katika kuboresha suala la ajira hapa nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali letu la mwisho, linatoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu, sasa aulize swali lake.

Na. 504

**Umwagiliaji Kutumia Chemchem ya Qang'dend – Mang'ola**

**MHE. QAMBALO W. QULWI** aliuliza:-

Eneo la Mang'ola katika bonde la Eyasi, Wilayani Karatu ni maarufu sana kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia chemchem za Qangded. Chemichemi hizo ziko katika hatari ya kutoweka kutokana na kuingiliwa na shughuli za kibinadamu:-

Je, ni lini Serikali itaweka mpango madhubuti wa uhifadhi wa chemchem hizo ikiwa ni pamoja na kuweka mipaka kwa kutumia sheria zilizopo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Bodi ya Maji ya Bonde la Kati kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu na Ofisi ya Katibu Tawala

Mkoa wa Arusha, mwaka 2017 ilifanya tathmini ya uharibifu wa mazingira, matumizi ya maji na mipaka ya chanzo hicho ambapo yafuatayo yalibainika:-

(1) Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha Qang'dend kimehifadhiwa kwa kuwekewa mpaka tangu mwaka 2006 na baadaye mwaka 2014 kwa umbali wa kuanzia mita 145 hadi mita 595 kulingana na eneo lilivyo katika maeneo yenye chemchem na umbali wa kuanzia mita 84 hadi mita 303 kwa baadhi ya maeneo ya kandokando ya Mto Mang'ola ambayo chanzo chake ni chemchem ya Qang'dend. Alama za mipaka zilizosimikwa haziheshimiki na wananchi katika baadhi ya maeneo kutokana na kwamba zingine zimejificha chini ya ardhi.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, pili, pampu zote za umwagiliaji zimeondolewa kwenye mto na kuwekewa nje ya mto kwenye umbali ambao hazina athari kwenye chanzo. Pia tathmini imebaini kuwa tatizo la chemchem kukauka limechangiwa na mchanga ama udongo mwingi uliosafirishwa kutoka maeneo ya juu ya chemchem na mito midogo iliyoingiza maji katika mto Mang'ola ambapo imesababisha kuziba kwa macho ya chemchem hizo.

(3) Mheshimiwa Naibu Spika, tatu; hatua zilizopangwa kutekelezwa na Wizara yangu ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji wa vyanzo, kuweka mipaka madhubuti katika maeneo yote muhimu ya chanzo na kuondoa michanga iliyoziba chemchem hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Willy Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu yasiyoridhisha kabisa ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, upimaji na uhifadhi wa chanzo cha maji cha Qang'dend si tu ni takwa la kisera na kisheria bali pia ilikuwa ni agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa

Majaliwa alipotembelea bonde la Eyasi mwishoni mwa mwaka 2016. Ni jambo la kushangaza kwa muda huo wote hadi sasa hatua hiyo ya uhifadhi haijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari sasa baada ya Bunge hili kwenda kutembelea vyanzo hivyo katika Bonde la Eyasi ili ashuhudie mwenyewe kwamba majibu aliyopewa si sahihi na achukue hatua stahiki kwa hawa ambao wametoa majibu hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swai la pili; kutokana na mvua nyingi zilizonyesha mwaka huu, chanzo hicho kimeharibika na kuathirika sana kutokana na mchanga kujazwa kwenye macho ya chemchem kiasi kwamba wananchi wenyewe wa Bonde la Eyasi wamejichangisha Sh.21,000,000 na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kutokana na mapato yake ya ndani imechan gia Sh.35,000,000 ili kuokoa vyanzo hivyo; lakini bado zinahitajika fedha zaidi ili kunusuru vyanzo hivyo. Je, Mheshimiwa Waziri, Wizara yake iko tayari sasa kuweka mkono ili kuunga mkono jitihada za wananchi hao? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru, lakini nipende kumjibu Mheshimiwa Mbunge; moja, ukirejea katika majibu ya swali lake la msingi tumeweka alama lakini baadhi ya alama hazionekani. Hata hivyo, kama Naibu Waziri wa Maji nataka nimhakikishie kwamba nipo tayari kufika katika Bonde la Eyasi na kujiridhisha katika haya majibu yametolewa ikitokea kwamba kuna udanganyifu kwa haya majibu, sichelei kusema watapata tabu waliondika haya majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali lake la pili, ni kuhusu suala zima la sisi kama Wizara kumuunga mkono. Waziri wangu amenipangia kufanya ziara katika mikoa mine, mojawapo ni Mkoa wa Arusha. Nataka nimhakikishie nikifika

katika eneo lile Mang'ola nitahakikisha namna gani tunaweza tukashauriana katika kuongeza nguvu zetu ili mwisho wa siku umwagiliaji katika chemchem ile uendelee na wananchi wake waendelee kuzalisha. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo swali fupi.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yamekuwa yakileta matumaini kwetu na kwa wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niulize swali. Wananchi wa Wilaya ya Nyasa waishio kando kando ya Ziwa Nyasa katika Vijiji vya Mkiri, Ngumbo na Ndumbi wana tatizo la kupata maji safi na salama. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wale wanapata maji safi na salama? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri na nia njema ya wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa sisi kama Wizara yetu ya Maji tulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kutuidhinishia fedha kiasi cha Sh.727,345,000,000; na utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Fedha hizi zipo nimwombe Mhandisi wa Maji ajipange sasa katika kuhakikisha wananchi wale wa vijiji ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge wanapata maji safi salama na yenye kutosheleza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu; nitaleta matangazo kwenu.

Tunao wageni wengi sana siku ya leo, kwa hivyo tunao wageni tunao hapa ndani kwa maana ya majukwaa tunayoyaona, lakini pia tunao wageni ambao wako ukumbi mwingi ambao wanaweza kutuona pia. Kwa hiyo tutawatangaza wageni hao kwa kadri tulivyoletewa hapa mbele.

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ni Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni wafugaji kutoka Wilaya ya Pangani Mkoani Tanga. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye ni Mhadhiri kutoka Sebastian Kolowa *Memorial University (SECOMU),* Chuo kilichopo Wilayani Lushoto Mkoani Tanga ambaye ni ndugu Alfred Walalaze. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 100 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, ambao ni Watoto wa *Sunday School* na Walimu wao wa Kanisa la *KKKT* Ipagala kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana watoto wa *Sunday School*. *(Makofi)*

Tunao vile vile wageni 48 wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Igunga Mkoani Tabora. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Tarime Mjini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 42 wa Mheshimiwa Silvestry Koka ambao ni viongozi wa *UVCCM* wakiongozwa na Mwenyekiti na Katibu wa *UVCCM* kutoka Kibaha Mjini Mkoani Pwani. Karibuni sana viongozi wa Chama cha Mapinduzi wa *UVCCM* kutoka Mkoani Pwani. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 30 wa Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga ambao ni viongozi mbalimbali kutoka Kata ya

Buigiri wakiambatana na Mshindi wa Ngoma za Asili Tanzania 2018, Ndg. Samwel Mandoo kutoka Buigiri, Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile kuna wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ambao ni wanafunzi na Walimu wa Chuo Kikuu cha *St. John's* kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu George Mpelumbe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni nane wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ambao ni Makatibu wa Mbunge na viongozi wa CCM kutoka Jimbo la Mufindi Mkoani Iringa. Karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi ambao ni wanafunzi wa kidato cha sita Shule ya Sekondari ya Wazazi ya Mwembetogwa kutoka Mkoani Iringa. Karibuni sana vijana wetu. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni wawili wa Mheshimiwa Cecilia Paresso ambao ni Madiwani kutoka Mkoani Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao vile vile wanafunzi 50 na Walimu watamp kutoka Shule ya Sekondari St. Mathew's ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani waliokuja kwa ajili ya mafunzo; karibuni sana Wanafunzi na Walimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wengine ambao wako kwenye ukumbi wetu mwingine tunaoita *basement*:-

Tutaanza na wageni 44 wa Mheshimiwa January Makamba ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, na hawa ni viongozi Wenyeviti na Makatibu wa CCM Kata za Jimbo la Bumbuli Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga. tutaanza na Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, yupo pia Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Lushoto, wapo pia Wenyeviti wa Kata wa CCM Bumbuli, wapo

Makatibu wa Kata wa CCM Bumbuli, wapo Makatibu wa Mbunge, yupo pia Katibu wa CCM Wilaya ya Lushoto. Viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilayani Lushoto, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Zainab Katimba ambaye ni ndugu Tizila Mahushi kutoka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Midimu ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dodoma anayeitwa Ndugu Jacob Christopher. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Justin Monko ambao ni marafiki zake na wadau wa maendeleo kutoka Mkoa wa Singida wakiongozwa na Ndugu Omari Mohamed Sombi. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Margaret Sitta ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Jimbo la Urambo wakiongozwa na Ndugu Josephat Ishengoma. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 48 wa Mheshimiwa Joel Makanyaga nadhani hili tangazo limerudi. Nadhani hili tangazo limerudiwa. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Daniel Mtuka ambao ni wenyeviti wa Vitongoji katika Wilaya ya Manyoni Mkoani Singida wakiongozwa na Ndugu Jackson Tadayo. *(Makofi)*

Tunae pia mgeni wa Mheshimiwa Joram Hongoli ambaye ni mdau wa habari kutoka Mkoani Njombe anaitwa Joftam Myefu. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi ambaye ni mtoto wake kutoka Musoma Mkoani Mara na yeye anaitwa Ndugu Wiliam Vedastus. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Rose Tweve ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Bernadetha Mushashu ambaye ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kakanja kutoka Kyerwa Mkoani Kagera, huyu ni Mwalimu Yelonimo Kihanga. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambaye ni Kiongozi wa UWT wa Kata kutoka Jijini Dodoma na huyu ni Ndg. Veronica Mabada. *(Makofi)*

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Aeshi Hilaly ambao ni wapigakura wake kutoka Jimboni kwake. *(Makofi)*

Pia wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni akina mama 100 kutoka Kanisa la *Redeem Assembly of God* kutoka mikoa mbalimbali wakiongozwa na Askofu Raphael Luvumbi. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo pia tangazo linalohusu ibada ya Misa kwa Wakristo wa Katoliki, kwamba mara baada ya kuahirishwa Bunge katika ukumbi wa Msekwa ghorofa ya pili ndiko ambako mtakutana. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenye ibada hiyo. Tangazo hili limeletwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas More Bunge Mheshiwa Shally Yosepher Raymond.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ratiba tuliyonayo kwenye hii karatasi yetu ya ratiba ama orodha ilikuwa leo tuwe na hoja mbele yetu ya Waziri Mpango ya kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018. Sasa kwa sababu tunaitarajia Kamati yetu ya Bajeti ituletee maoni ya Waheshimiwa Wabunge wanaotuwakilisha huko, Kamati yetu imetutaarifu kwamba inaendelea na hiyo kazi na Waziri

yuko huko ili waweze kukamilisha. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge hatutaendelea na hii ratiba kwa leo.

Waheshimiwa Wabunge, niseme jambo moja kabla sijaahirisha Bunge, wageni wetu wale maafisa mnao waongoza wakati matangazo yakisomwa hapa mbele wageni hawaruhusiwi kusimama na kutembea wala kutoka nje. Wanapaswa wasubiri aidha, nikae au niahirishe Bunge ndiyo watoke nje, ndiyo utaratibu, haruhusiwi mtu kusimama wakati mimi nimesimama. Kwa hiyo, wageni mkiwa mnawatoa wakati tunaendelea na matangazo mnakuwa mnazikosea kanuni zetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mnaokuwa na Wageni lakini pia Maafisa wetu wanaoongoza wageni wawaongoze vizuri, hawaruhusiwi kusimama anayeongoza hapa akiwa amesimama ndizo taratibu zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho asubuhi saa tatu kamili.

*(Saa 4.52 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 28 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*